**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA, KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA OFISI HIYO MWAKA WA FEDHA 2019/2020

---

[*Imetolewa chini ya Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016]*

Ofisi ya Bunge
S.L.P 941
**DODOMA**

APRILI, 2019

## YALIYOMO


1.0 UTANGULIZI ......................................................................................1
2.0 TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 ............................4
2.1 Ufafanuzi wa Miradi ya Maendeleo iliyokaguliwa ................................................4
2.1.1 Mradi Na. 4921 - Mpango wa Kurasimisha Raslimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA). ..................................................................5
2.1.2 Mradi Na. 6220 – Support to Tanzania Social Action Fund (TASAF)......................7
2.1.3 Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC) ..................................................................9
2.2 Matokeo ya Ukaguzi ...........................................................................................10
2.2.1 Mradi Na. 4921 - Mpango wa Kurasimisha Raslimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) .................................................................10
2.2.2 Mradi Na. 6220 – Support to Tanzania Social Action Fund (TASAF) - Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini ................................................................13
2.2.3 Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC) ...............................................................17
3.0 MAONI YA JUMLA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 ...............................................................20
4.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAPENDEKEZO YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 ..............................................................................................22
4.1 Uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ..........................................................................................22
4.2 Upatikanaji wa fedha kutoka Hazina ..................................................................22
4.3 Mapitio ya Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati ....................................25
5.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020 ...............................................................28
5.1 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020..............28
5.2 Uchambuzi wa Bajeti ya Wizara kwa kulinganisha na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka wa Fedha 2019/2020.......................................34
6.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI ...................................................................39
7.0 HITIMISHO.........................................................................................................43

# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA, KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA, KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA OFISI HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa mwaka wa fedha 2018/2019, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa Fedha 2019/2020.

Kifungu cha 6 (4)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, kimeipa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa jukumu la kusimamia shughuli za Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Aidha, Kifungu cha 7(1) (a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, kinatoa wajibu kwa Kamati zote za Kisekta kushughulikia bajeti za Wizara zinazozisimamia. Jukumu hili la uchambuzi wa bajeti ambalo hutekelezwa kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za Bunge, hutanguliwa na jukumu la ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha unaoisha kwa mujibu wa Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, ilifanya ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo katika mikoa ya Lindi na Mtwara, iliyotengewa na kupokea fedha katika mwaka wa fedha 2018/2019 kuanzia tarehe 12 hadi 17 Machi, 2019. Kamati pia ilifanya uchambuzi wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora tarehe 18 na 19 Machi, 2019.

Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ina Mafungu Nane (8) ya bajeti kama ifuatavyo:-

i) **Fungu 20:** Ofisi ya Rais, Ikulu;
ii) **Fungu 30:** Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri;
iii) **Fungu 32:** Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma;
iv) **Fungu 33:** Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma;

v) **Fungu 67:** Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma;

vi) **Fungu 94:** Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma;

vii) **Fungu 09:** Ofisi ya Rais, Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma; na

viii) **Fungu 04:** Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa

**Mheshimiwa Spika,** taarifa hii inatoa maelezo kuhusu maeneo manne yafuatayo:-

i) Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotembelewa na Kamati;

ii) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa Fedha 2018/2019;

iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii kwa mwaka wa Fedha 2019/2020; na

iv) Maoni na Ushauri wa Kamati.

## 2.0 TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

### 2.1 Ufafanuzi wa Miradi ya Maendeleo iliyokaguliwa

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2018/2019, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ilitengewa **shilingi 195,973, 361, 000/=** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kupitia mafungu matano kama ifuatavyo:-

i) **Fungu 30:** Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri – **Tshs. 175,055,489,000/=**;

ii) **Fungu 32:** Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma – **Tshs. 10,939,000,000/=**;

iii) **Fungu 33:** Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma – **Tshs. 4,050,000,000/=**;

iv) **Fungu 67**: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma - **Tshs. 750,000,000/=**; na

v) **Fungu 4:** Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa – **Tshs. 5, 178,872,000/=**.

**Mheshimiwa Spika,** katika kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari 2016, Kamati ya

Utawala na Serikali za Mitaa, ilitembelea baadhi ya miradi iliyotekelezwa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Miradi iliyotembelewa ni ile inayotekelezwa chini ya Mpango wa Kurasimisha Raslimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA), Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) na Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania (TPSC). Ufafanuzi kuhusu miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

2.1.1 **Mradi Na. 4921 - Mpango wa Kurasimisha Raslimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA).**

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu ulitengewa **Shilingi 1,500,000, 000/=** na unatekelezwa chini ya Kifungu 1003 *"Policy and Planning"* cha **Fungu 30** – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri.

Mpango huu unatekeleza jukumu la kuandaa na kusimamia mfumo wa kitaifa wa umiliki wa raslimali na uendeshaji wa biashara nchini kwa mujibu wa sheria. Mpango huu umewezesha wanyonge kurasimisha ardhi na biashara na kuvitumia kama dhamana ya kupata mikopo ambayo imewawezesha kukuza mitaji ya shughuli za kiuchumi.

Taarifa zilizowasilishwa kwenye Kamati zilibainisha kwamba, MKURABITA imewajengea wakulima 362 na viongozi 88 wa vyama

vya wakulima uwezo wa kutumia Hati za Haki Miliki za Kimila kupata mitaji katika benki na taasisi zingine za fedha katika halmashauri za wilaya za Mvomero na Magu. Kutokana na mafunzo hayo, wakulima 100 wameweza kufungua akaunti katika benki mbalimbali.

Aidha, vituo viwili vya urasimishaji wa biashara (*one stop formalization centre*) vimeanzishwa katika Halmashauri ya Mji wa Njombe na Halmashauri ya Manispaa ya Singida, ambapo huduma muhimu za utoaji wa leseni za biashara, namba ya utambulisho wa mlipa kodi (TIN), ujasili wa jina la biashara (BRELA), huduma za kibenki na mifuko ya hifadhi ya jamii zinapatikana. Aidha, wafanyabiashara 1,527 wamepata mafunzo ya urasimishaji na uendeshaji wa biashara na katika kipindi hicho vituo hivyo vimesajili biashara 738 na wafanyabiashara 400 wamefungua akaunti katika benki kwa ajili ya kuweka akiba na kukopa fedha ili kuongeza mitaji.

Kwa upande wa Zanzibar urasimishaji wa biashara katika wilaya za Magharibi A, Unguja na Mkoani Pemba umeanza ambapo wafanyabiashara 100 watapata mafunzo na kusajiri biashara zao.

Aidha, kwa kushirikiana na Ofisi za Taifa za Takwimu, Tanzania Bara na Zanzibar, MKURABITA imefanya utafiti kuhusu sekta isiyo rasmi nchini kwa lengo la kubaini ukubwa na thamani ya sekta hiyo na maandalizi ya ripoti yako katika hatua ya ukamilishaji. Maeneo yaliyohusika katika utafiti huo ni mikoa ya Mbeya, Mwanza, Dodoma,

Dar es Salaam, Tanga na Mtwara kutoka Tanzania Bara na Mjini Magharibi na Kusini Pemba, kutoka Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,** vilevile MKURABITA imeingia makubaliano na Benki ya NMB kwa ajili ya utekelezaji wa miradi majaribio ya Mfuko Endelevu wa Urasimishaji wa Wilaya. Utekelezaji umeanza katika Manispaa ya Iringa ambapo Serikali imeweka fedha za dhamana katika benki ya NMB ili kuziwezesha halmashauri kukopa na kuendesha shughuli za urasimishaji endelevu.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa Kamati ilitembelea Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea, Mkoani Lindi ili kujiridhisha kuhusu hali ya utekelezaji wa MKURABITA.

### 2.1.2 Mradi Na. 6220 – Support to Tanzania Social Action Fund (TASAF)

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu ulitengewa jumla ya **Shilingi 74,360,989,000** na ulipangwa kutekelezwa chini ya Kifungu 1003" *Administration and Human Resource Management"* cha **Fungu 30** – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri.

Mfuko huu unatekelezwa katika mamlaka zote za Serikali za Mitaa Tanzania Bara na Wilaya zote za Zanzibar, na uko katika awamu ya tatu ya utekelezaji wake ambayo inasaidia kaya maskini za watanzania kukuza uchumi na hivyo kupunguza umaskini wa kipato;

kuinua ubora wa maisha na ustawi wa jamii, na kuhamasisha uwajibikaji na kuzingatia utawala bora.

Taarifa ya utekelezaji inaonesha kuwa, tangu kuanza kutekelezwa kwa awamu ya tatu ya TASAF takribani kaya maskini 1,007,588 zenye jumla ya watanzania **Milioni 5** zimeandikishwa na kunufaika.

Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2018 hadi Februari, 2019 kiasi cha **Shilingi Bilioni 135** kilitolewa kama ruzuku kwa idadi hiyo ya kaya ambayo inajumuisha Vijiji/Mitaa/Shehia 9,960 kutoka pande zote za Muungano.

**Mheshimiwa Spika**, taarifa zilibainisha kuwa mpango huu umetoa ajira kwa kaya za walengwa 288,837 kutokana na utekelezaji wa miradi 3,043 yenye thamani ya **Shilingi bilioni 14.2**. Miradi hiyo inatekelezwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 42 na Wilaya zote za Zanzibar kwa kuhusisha Vijiji/Mitaa na Shehia 2,590.

Aidha, zoezi la uhakiki kwa lengo la kuondoa kaya zisizo na sifa kwenye mpango, liliendelea katika kipindi hicho cha kuanzia Julai, 2018 hadi Februari, 2019 ambapo kaya 4,840 ziliondolewa kutokana na kukosa sifa au vigezo. Miongoni mwa sababu za kaya hizo kupoteza sifa ni pamoja na mwanakaya au wanakaya kufariki, kaya kuhamia maeneo ambapo mpango haujaanza kutekelezwa au kaya kushindwa kujitokeza kupokea ruzuku mara mbili mfululizo.

Vilevile, TASAF imeandaa malipo kwa walengwa kwa njia ya kielektroniki kupitia mitandao ya simu na benki na majaribio kufanyika katika mamlaka za maeneo ya utekelezaji 16 ambazo ni Jiji la Arusha, Manispaa za Temeke, Kinondoni, Ilala, Kigoma Ujiji, Songea, Halmashauri za Bahi, Siha, Kilwa, Bagamoyo, Kisarawe, Mkuranga, Urambo, Muheza, Mpanda Mji na Halmashauri zote za Unguja na Pemba kwa upande wa Zanzibar. Hadi kufikia mwezi Februari, 2019 **Shilingi bilioni 16.2** zililipwa kwa walengwa 55,763.

**Mheshimiwa Spika,** ili kujiridhisha kuhusu utekelezaji wa mpango huu Kamati ilitembelea na kukagua Kijiji cha Namela kilichopo Kata ya Msanga Mkuu, Tarafa ya Ziwani, Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara, Mkoani Mtwara.

### 2.1.3 Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC)

**Mheshimiwa Spika,** chuo hiki kilianzishwa kwa lengo la kutoa mafunzo, ushauri na kufanya utafiti tumizi na kutoa machapisho mbalimbali katika nyanja za uongozi, menejimenti na utawala. Aidha, chuo kinaendesha kozi za kitaaluma kwa ngazi ya astashahada, stashahada na shahada katika nyanja za Uhazili, Utunzaji Kumbukumbu, Menejimenti ya Raslimali Watu, Utawala na Manunuzi ya Umma. Chuo kinatekeleza majukumu hayo katika Kampasi Sita (6) zilizoko katika Mikoa ya Dar es Salaam, Tabora, Tanga, Singida, Mbeya na Mtwara.

Vile vile, chuo kiko mbioni kuanzisha Kampasi ya Dodoma ambapo jengo limepatikana na ukarabati utaanza muda si mrefu ili kuliwezesha kuwa katika hali bora ya kutumika kwa mahitaji ya chuo. Ili kujiridhisha kuhusu utendaji wa chuo hiki, Kamati ilitembelea Kampasi ya Mtwara ili kupata taarifa na kukagua mazingira ya chuo.

## 2.2 Matokeo ya Ukaguzi

**Mheshimiwa Spika,** ili kuwezesha tija ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha chini ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa mwaka wa fedha unaoisha, upo umuhimu wa kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuhusu yaliyojiri kutokana na ukaguzi huo. Kwa madhumuni hayo taarifa hii imetumia njia kadhaa ikiwa ni pamoja na asilimia, majedwali, ulinganishaji na utofautishaji ili kubainisha hali ya utekelezaji wa miradi iliyo chini ya Ofisi hii. Ufafanuzi wa matokeo ya ukaguzi huo ni kama ifuatavyo: -

### 2.2.1 Mradi Na. 4921 - Mpango wa Kurasimisha Raslimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA)

**Mheshimiwa Spika,** katika Halmashauri ya Nachingwea Kamati ilipokea taarifa za utekelezaji wa mpango huu katika Vijiji vya Mbondo, Nahimba na Nakalonji, ambavyo kutokana na mafunzo ya

vitendo jumla ya mashamba 2,328 yameweza kupimwa na Hati za Haki Miliki za Kimila 2180 kuandaliwa.

Aidha, MKURABITA imewezesha Vijiji 104 kati ya 127 katika halmashauri hiyo kupima mipaka yake na kuandaa mpango wa matumizi ya ardhi hadi sasa.

Kamati ilitembelea na kukagua utekelezaji wa MKURABITA, katika Kijiji cha Mbondo ambapo upimaji wa mashamba 1,304 ulifanyika na jumla ya hati 750 kuandaliwa. Katika ziara hiyo mambo kadhaa yalibainika ikiwa ni pamoja na mafanikio na changamoto. **Jedwali Na. 01** linatoa muhtasari wa hali ya utekelezaji wa mpango huu katika Halmashauri ya Nachingwea.

**Jedwali Na. 01: Mashamba yaliyopimwa katika Halmashauri ya Nachingwea, Mkoani Lindi**

| Na. | Kijiji | Mashamba yaliyopimwa | Hati zilizotolewa | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Mbondo | 1304 | 750 | 57.52 |
| 2. | Nahimba | 505 | 341 | 67.52 |
| 3. | Nakalonji | 519 | 256 | 49.33 |
| **Jumla** | | **2328** | **1341** | **57.69** |

**Chanzo:** Taarifa za MKURABITA kuhusu urasimishaji wa ardhi na biashara.

**Mheshimiwa Spika,** mafanikio na changamoto vilivyobainika kutokana na urasimishaji ni pamoja na:-

**(a) Mafanikio**

i) Kupungua kwa migogoro ya matumizi ya ardhi na mipaka ya miliki katika vijiji husika;

ii) Kuongezeka kwa usalama wa milki ya ardhi kwa wananchi waliorasimisha ardhi yao;

iii) Wanawake wamepata fursa ya ama kumiliki Hati za Haki Miliki ya ardhi peke yao au kwa kushirikiana na Waume zao;

iv) Baadhi ya wananchi wamekuza mitaji ya kiuchumi kutokana na kutumia Hati za Haki Miliki za Kimila kama dhamana ya kupata mikopo katika benki na taasi nyingine za kifedha;

v) Mafanikio katika vijiji vilivyotekeleza urasimishaji yamekuwa chachu ya kuendeleza zoezi hilo katika Vijiji 24 ambapo mashamba 251 yamepimwa na utaratibu wa kuandaa hati unaendelea; na

vi) Kuongezeka kwa thamani ya ardhi ya wananchi katika maeneo yaliyorasimishwa.

**(b) Changamoto**

i) Uhaba wa fedha unahafifisha utekelezaji wa MKURABITA katika maeneo mengine ya Halmashauri ya Nachingwea;

ii) Halmashauri inashindwa kuendeleza urasimishaji hata baada ya watendaji wake kujengewa uwezo wa kimafunzo na MKURABITA;

iii) Ukosefu wa Wataalam wa kuandaa na kusajili Hati za Haki Miliki za Kimila, jambo linalochelewesha kukamilika kwa hati hizo. Kutokana na kukosekana kwa Afisa Ardhi Mteule, hati hizo zinalazimika kupelekwa Halmashauri za Ruangwa au Masasi kwa ajili ya maandalizi na usajili;

iv) Baadhi ya Wananchi kushindwa kugomboa Hati za Haki Miliki za Kimila za maeneo waliyopimiwa;

v) Wamiliki wa Hati za Haki Miliki za Kimila kukosa ujuzi wa kuandaa maandiko ya miradi ambayo yatawawezesha kupata mikopo kutoka benki na taasisi nyingine za kifedha; na

vi) Wamiliki wa mashamba kuuza kiholela mashamba yao baada ya upimaji na hivyo kukwamisha zoezi la utoaji Hati za Haki Miliki za Kimila kutokana na upimaji wa awali.

### 2.2.2 Mradi Na. 6220 – Support to Tanzania Social Action Fund (TASAF) - Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitembelea Kijiji cha Namela kilichopo Wilayani Mtwara ambacho ni miongoni mwa vijiji 99 vinavyonufaika na mpango wa kunusuru kaya maskini katika Wilaya hiyo. Kijiji hiki

kina jumla ya Kaya 117 zinazonufaika na mpango huu. Kaya hizo zimepokea ruzuku ya **shilingi milioni 109.99** kutokana na awamu 30 za uhawilishaji tangu kuanza kwa mpango huo Julai – Agosti, 2014 hadi Januari – Februari, 2019.

Aidha, TASAF imewezesha Kijiji cha Namela kutekeleza miradi ya utoaji wa ajira za muda kwa kaya zote 117 za walengwa kwa kugharamia mradi wa upandaji wa mikoko katika eneo la ufukwe wa Bahari ya Hindi lenye ukubwa wa ekari 4 kwa gharama ya s**hilingi milioni 14.46** na ujenzi wa kisima cha pete kwa gharama ya **shilingi milioni 14.89**. Jumla ya **shilingi milioni 7.12** zilitumika kwa ajili ya ununuzi wa vifaa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo.

Vile vile, kupitia mpango wa kuweka akiba na kukuza uchumi wa kaya ambao unalenga kuziwezesha kaya zilizo katika mpango wa kunusuru kaya maskini kuwa na uwezo wa kukuza mitaji kwa ajili ya shughuli za kiuchumi ili kuongeza kipato, kuona umuhimu wa vikundi na umuhimu wa kuweka akiba katika kaya, jumla ya vikundi 8 vya kuweka akiba za kukuza uchumi wa kaya vimeundwa. Hadi Kamati inatembelea kijijini cha Namela **shilingi milioni 2.98** zilikuwa zimewekwa kama akiba ya vikundi hivyo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilishuhudia namna ambavyo baadhi ya wanufaika wa mpango wametumia fedha za ruzuku kujenga na kuboresha makazi yao. Miongoni mwa wanufaika hao ni Bw. Abdallah Ismail Hamadi Tungwalu (65) na Bi. Fatuma Shamte Abdallah (81),

ambao wametumia ruzuku wanayoipata kuwa chachu ya kujenga na kuboresha makazi pamoja na hali ya uchumi wa familia.

Bi. Fatuma Shamte Abdallah, ambaye ni mjane anayeishi na wajukuu zake wawili anaeleza kwamba, mpango wa ruzuku umemuwezesha kuboresha hali ya maisha kwa kuendesha ufugaji wa mbuzi na kuku.

Wajumbe wa Kamati walishuhudia nyumba bora ambayo inajengwa na Bi. Fatuma kwa kutumia saruji, mawe na mchanga. Akiongea kwa kujiamini Bi. Fatuma anasema, "***TASAF ndiye bwana angu. Mimi na wajukuu wangu tumetoka kula mlo mmoja, hadi sasa tunakula milo mitatu. Ninavaa kitenge kizuri, wajukuu zangu wanasoma bila hofu kwani wanapata mahitaji muhimu ya Shule".***

Kwa upande wake Mzee Hamad anasema ruzuku ya kaya maskini ilimuwezesha kuwa mfugaji wa mbuzi kwa kuanza na mbuzi wawili (2) tu, lakini sasa wamefika 17. Aidha, kupitia mpango huo mbali na kumudu milo mitatu kwa siku, anatekeleza ujenzi wa nyumba ya matofali na saruji ambayo iko katika hatua ya renta.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na ukaguzi huo, Kamati ilibaini mambo yafuatayo: -

**a) Mafanikio;**

i) Kuongezeka kwa kiwango cha mahudhurio ya watoto shuleni hasa wanaotoka kaya za walengwa, tofauti na awali. Hii inatokana na kukua kwa uchumi na kipato cha kaya kupitia ruzuku na shughuli za mpango kwa watoto wanaosoma shule;

ii) Kaya zote 117 za walengwa katika Kijiji cha Namela zimejiunga na huduma ya Bima ya Afya ya Jamii (CHF) na hivyo kuwezesha walengwa kupata huduma za afya kutoka vituo vya kutolea huduma kwa gharama nafuu;

iii) Kaya za walengwa zimeboresha makazi kwa kukarabati makazi ya awali au kujenga mapya kutokana na fedha za ruzuku. Jumla ya Kaya 67 za walengwa zimeboresha makazi. Idadi hiyo ni sawa na asilimia 57.26 ya kaya zote za walengwa 117;

iv) Kuongezeka kwa mahudhurio ya kliniki kwa watoto walio chini ya miaka mitano kutoka kaya za walengwa kutokana na kaya kupata ruzuku ya kuboresha na kujenga afya ya mtoto na ukuaji wake;

v) Watoto kutoka kaya za walengwa wanapata mahitaji muhimu ya shule kutoka kwa wazazi kama vile sare, kalamu na madaftari;

vi) Walengwa wa mpango wametumia sehemu ya ruzuku kuanzisha miradi ya kiuchumi kama vile, ufugaji, kilimo,

na biashara na kuongeza kipato ambacho kimewasaidia kuboresha maisha; na

vii) Kupungua kwa ajira za watoto wadogo kwani sasa wanahudhuria Shule.

**b) Changamoto;**

i) Ushirikiano hafifu kutoka kwa watoa huduma za afya na elimu, ambao husababisha ugumu katika kupata taarifa za watoto wa walengwa wanaopata huduma katika maeneo husika;

ii) Malalamiko kutoka kaya maskini ambazo hazijaingizwa kwenye mpango;

iii) Kuchelewa kwa vifaa vya mpango wa kuweka na kuwekeza katika vikundi vilivyoundwa na walengwa na hivyo kusababisha vikundi kutunza fedha katika mazingira yasiyo salama;

iv) Baadhi ya wanakamati wa CMC kulalamikia ujira/posho kidogo wanayoipata; na

v) Baadhi ya wananchi kukosa uelewa wa kutosha kuhusu utekelezaji wa mpango.

### 2.2.3 Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC)

**Mheshimiwa Spika,** chuo hiki kilianzishwa rasmi kama Wakala wa Serikali, Agosti, 2000 kwa Sheria ya Wakala za Serikali Na. 30 ya

Mwaka 1997, baada ya kuunganishwa kwa vyuo viwili, Chuo cha Watumishi wa Serikali (*Civil Service Training Centre*) kilichokuwa Dar es Salaam na Chuo cha Uhazili Tabora *(Tabora Secretarial College*).

Uanzishwaji wa chuo hiki ulilenga kusaidia maboresho katika Utumishi wa Umma ili kuwe na matokeo na tija katika utoaji wa huduma.

**Mheshimiwa Spika,** tangu kuanzishwa kwake, chuo ambacho ni nguzo muhimu ya mafunzo ya kiutumishi kwa Watumishi wa Umma nchini, kimeweza kuongeza matawi hadi kufikia sita ambayo yako katika Mikoa ya Dar es Salaam, Mtwara, Singida, Mbeya, Tabora na Tanga. Katika ziara yake, kwenye Kampasi ya Mtwara Kamati ilibaini mambo yafuatayo:-

**(a) Mafanikio**

i) Tawi lilidahili watumishi 20 kwenye Mitihani ya Serikali (PSE) na watumishi 287 kwenye mafunzo ya muda mfupi;

ii) Tangu mwaka 2009, tawi limetoa wahitimu 8,560 katika fani mbalimbali kwa ngazi za astashahada na stashahada;

iii) Tawi limepunguza watumishi wa mikataba kutoka asilimia 76 hadi asilimia 41;

iv) Tawi limepata usajili kamili kutoka Baraza la Ithibati la Elimu ya Ufundi Tanzania (NACTE); na

v) Tawi linamiliki viwanja (Plot Na. 47 na 49) katika eneo la Shangani. Hii ni tofauti na Kampasi nyingine ambazo zinatumia majengo ya kupanga;

**(b) Changamoto**

i) Tawi linakabiliwa na uhaba wa mabweni, jambo linalokwamisha ongezeko la udahili wa wanafunzi;

vi) Tawi lina upungufu wa vitabu 200 ambavyo vingewezesha kuwa na uwiano mzuri kati ya mwanafunzi na vitabu;

vii) Majengo matatu ya tawi (Block A, B, na C) yameanza kuchoka na kumomonyoka, na hivyo kuhatarisha usalama wa watumiaji; na

viii) Mwitikio hafifu kutoka Wizara na Taasisi za Umma katika kutumia huduma za Chuo hicho.

## 3.0 aoni ya Jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2018/2019

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na matokeo ya ukaguzi wa miradi ya Maendeleo, ni maoni ya Kamati kwamba: -

i) Wanufaika wa mpango wa ruzuku kwa kaya maskini wanaweza kujikwamua kiuchumi iwapo watatumia sehemu ya ruzuku kuanzisha miradi midogo midogo ya kiuchumi kama vile biashara, ufugaji au kilimo. Aidha, Idara ya Maendeleo ya Jamii katika halmashauri isaidie kuwaelimisha walengwa hao;

ii) Iwapo TASAF itahakiki na kusajili kaya maskini zilizosahaulika katika mpango wa ruzuku kwa kaya maskini, itasaidia kupunguza au kuondoa malalamiko miongoni mwa wanajamii;

iii) Mpango wa ruzuku kwa kaya maskini umechangia kuboresha mahudhurio ya watoto wa kaya maskini shuleni na kliniki;

iv) Bajeti finyu kwa MKURABITA inaathiri utendaji wa mpango huo na hivyo kukwamisha zoezi la urasimishaji;

v) Watendaji wa halmashauri waliojengewa uwezo na MKURABITA, wanaweza kuendeleza zoezi la urasimishaji iwapo watawezeshwa kwa kupatiwa vifaa na raslimali fedha;

vi) Benki na Taasisi za fedha zikielimishwa kuhusu hadhi ya Hati za Hakimiliki za Kimila kutumika kama dhamana ya mikopo, zitatoa mikopo kwa wananchi wanaomiliki ardhi kwa hati hizo;

vii) Halmashauri zikipatiwa Wataalam wa Ardhi, zitasaidia MKURABITA kuharakisha zoezi la kurasimisha ardhi na kutoa Hati za Hakimiliki kwa wahusika; na

viii) Iwapo Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania, Kampasi ya Mtwara kitawezeshwa kumiliki viwanja Na. 41 na 46 vilivyo jirani na kampasi hiyo, kitaweza kujenga mabweni na hivyo kuondoa usumbufu kwa wanafunzi wanaolazimika kupanga vyumba mbali na chuo.

## 4.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAPENDEKEZO YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

### 4.1 Uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2018/2019

**Mheshimiwa Spika,** katika kuchambua Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa mwaka wa fedha 2018/2019 Kamati ilijikita katika kuangalia mwenendo na upatikanaji wa fedha za matumizi kwa ajili ya shughuli zilizopangwa.

Njia kubwa zilizotumiwa na Kamati wakati wa uchambuzi huu ni pamoja na kuangalia hali halisi, kuzingatia taarifa mbalimbali zilizowahi kuwasilishwa kwenye Kamati na mahojiano yaliyochangia upatikanaji wa taarifa muhimu wakati wa vikao vya Kamati.

### 4.2 Upatikanaji wa fedha kutoka Hazina

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, umebaini kwamba hakuna ulinganifu kati ya kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa mwaka wa fedha 2018/2019 na kiasi kinachotolewa na Hazina. Kutokana na uchambuzi huo, Kamati imebaini kuwa:-

i) Fedha zilizoidhinishwa zinatolewa kidogo ikilinganishwa na mpango wa upatikanaji fedha (cash flow plan);

ii) Fedha za matumizi ya kawaida zinatolewa kwa kiasi kikubwa ikilinganishwa na fedha za maendeleo (matumizi ya kawaida asilimia 76 na maendeleo asilimia 46);

iii) Fedha hazipatikani kwa wakati na hivyo kuathiri utekelezaji wa malengo ya Bajeti ya Ofisi hii.

Maelezo hayo ni matokeo ya ulinganisho wa fedha zilizopokelewa na mafungu yaliyo chini ya Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kutoka hazina hadi kufikia mwezi Februari, 2019 (robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2018/2019) na kiasi cha fedha kilichoidhinishwa.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi zaidi umebainisha kwamba, hadi kufikia mwezi Februari, 2019 Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi

wa Umma na Utawala Bora, pamoja na mafungu yaliyo chini yake, ilikuwa imepokea jumla ya **shilingi 374, 706, 943, 857/=** kutoka Hazina kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo. Kiasi hicho ni sawa na **asilimia 65.03** ya fedha yote iliyoidhinishwa na Bunge.

Kiasi hicho cha fedha kimepungua kwa takribani **shilingi 43,072,387,704** (sawa na asilimia **10.31)** ikilinganishwa na kiasi kilichopatikana katika kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2017/2018 ambacho kilikuwa ni **shilingi 417,779,331,561**.

Kwa upande wa fedha za maendeleo uchambuzi umeonesha kwamba, hadi kufikia mwezi Februari, 2019, Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na mafungu yake, ilikuwa imepokea jumla ya **shilingi 82,052, 427,230/=** kutoka hazina, sawa na **asilimia 46. 87** ya fedha yote iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya maendeleo.

Kiasi hicho cha fedha ni pungufu kwa **asilimia 60.31** ikilinganishwa na kiasi kilichopokelewa kwa kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2017/18 kwa ajili ya maendeleo ambacho kilikuwa ni **shilingi 206,720,967,511/=**.

Aidha, imebainika kwamba, kwa ujumla mwenendo wa upatikanaji wa fedha haukuwa mzuri, kwani fedha zilizopatikana zilikuwa ni takribani **asilimia 65.03** ya fedha zote zilizoidhinishwa. Kwa tafsiri rahisi ni kwamba, kiasi cha asilimia 25 kilichopaswa kupatikana kwa kila robo ya mwaka wa fedha hakikuweza kupatikana. Kwa kuzingatia kiasi hicho ilitarajiwa kwamba hadi kipindi hicho kiasi cha fedha

kilichoidhinishwa kilipaswa kuwa kimepatikana kwa takribani **asilimia 70**.

Vilevile, katika kipindi hicho jumla ya **shilingi 292,654,516,627/=** zilikuwa zimepokelewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, sawa na **asilimia 72.95** ya fedha iliyoidhinishwa kwa ajili hiyo. Tafsiri ya mwenenendo huo ni kwamba, kiasi hicho ni pungufu kwa takribani asilimia 1.99 ikilinganishwa na **shilingi 298,604,842,833** zilizopokelewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida katika kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2017/2018.

Hali hiyo inaweza kutafsiriwa kwamba, kiasi cha fedha za matumizi ya kawaida kinachotolewa na hazina kimeendelea kuwa kikubwa ikilinganishwa na fedha za maendeleo. Hali hii imejitokeza kwa miaka mitatu ya fedha mfululizo tangu mwaka 2016/17 hadi 2018/19.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla uchambuzi umebaini kwamba, mtiririko wa fedha kutoka hazina siyo mzuri ikilinganishwa na miaka iliyopita kwani, kiasi kinachotolewa kimeendelea kupungua mwaka hadi mwaka huku fedha za maendeleo zikiwa pungufu zaidi ya zile za matumizi ya kawaida.

## 4.3 Mapitio ya Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa kupitia na kuchambua Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Kamati ilitoa ushauri katika mambo

Kumi na Saba (17) kwa lengo la kuhakikisha bajeti hiyo inatekelezwa kwa ufanisi.

Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, imezingatia kikamilifu baadhi ya maoni na ushauri wa Kamati na inaendelea kuzingatia yaliyosalia. Baadhi ya maoni na ushauri vilivyozingatiwa ni kuhusu:-

i) Serikali kupunguza urasimu katika kuthibitisha Watumishi wa nafasi za uteuzi, ambapo iliweza kuidhinisha asilimia 81 ya nafasi za uteuzi zipatazo 1,332 na taratibu za uteuzi zinaendelea;

ii) Serikali kupitia Taasisi ya Uongozi (Uongozi Institute) itoe mafunzo ya uongozi na utawala kwa viongozi wanaoteuliwa ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Miongozo ya kiutendaji na hivyo kuepusha migongano isiyo ya lazima ambayo inaweza kuibuka. Mafunzo yalitolewa kwa wakurugenzi wa serikali za mitaa, wakuu wa wilaya, wakuu wa mikoa na makatibu tawala wa mikoa na wlaya;

iii) Benki na Taasisi za fedha zielimishwe kuhusu hadhi ya Hati za Haki Miliki za Kimila kutumika kama dhamana ya mikopo, ambapo baadhi ya benki na taasisi za fedha zimeanza kukubali hati hizo baada ya kuelimishwa. Aidha, wananchi zaidi ya 500

wametumia hati hizo kukopa **shilingi bilioni 4.9** kutoka Benki za CRDB, NMB, PSPF na Agricultural Inputs Trust Fund. Vilevile, vyama vya wakulima vimedhamini wakulima kukopa jumla ya **shilingi milioni 625.9;**

iv) Kutambua na kuandikisha Kaya maskini katika maeneo ya Vijiji 4,408, Mitaa 1,189 na Shehia 96 ambayo hayakufikiwa katika awamu ya kwanza ya mpango wa ruzuku kwa kaya maskini, ambapo maandalizi ya awamu ya pili ya utekelezaji wa TASAF III yako katika hatua za mwisho na maeneo yote hayo yatafikiwa; na

v) Watendaji wa Halmashauri washirikiane na MKURABITA, katika kuandaa na kutekeleza mpango bora wa matumizi ya ardhi na hivyo kupunguza au kuepusha migogoro ya ardhi baina ya makundi ya watumiaji katika jamii; ambapo zoezi hilo linatekelezwa katika Halmashauri za Misungwi, Mpwapwa na Serengeti.

## 5.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

### 5.1 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa fedha 2019/2020, Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, inayojumuisha Mafungu Nane (20; 30; 32; 33; 67; 94; 09 na 04) imeandaliwa kwa kuzingatia vipaumbele vilivyoanishwa katika:-

i. Ilani ya Uchaguzi ya Mwaka 2015 ya Chama Tawala,
ii. Mwongozo wa Taifa wa Kuandaa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2019/2020, pamoja na
iii. Maeneo muhimu ya kuzingatiwa kama yalivyoanishwa na Serikali ya Awamu ya Tano.

Kwa ujumla ofisi hii pamoja na mafungu yake imepanga kutekeleza malengo **177** katika mwaka wa fedha ujao malengo hayo ni pamoja na:-

i) Kutoa huduma kwa Rais na familia yake;

ii) Kutoa huduma za ushauri kwa Rais katika maeneo ya uchumi, siasa, masuala ya jamii, sheria, mawasiliano na

habari kwa umma, mahusiano ya kikanda, kimataifa na maeneo mengine;

iii) Kuratibu utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Tatu (NACSAP III) kwa kushirikisha wadau wa sekta ya umma na sekta binafsi;

iv) Kuratibu,kuandaa na kushiriki mikutano 60 ya Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri, mikutano 40 ya Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu (IMTC) na Mikutano 20 ya Baraza la Mawaziri;

v) Kuratibu na kusimamia miradi ya maendeleo ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) na Mpango wa Kurasimisha Raslimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA);

vi) Kuendelea na uboreshaji wa Ikulu ya Chamwino, na kukarabati majengo ya ikulu ndogo za Mwanza; Arusha, Mbeya, Zanzibar, Lushoto na nyumba mbili za wafanyakazi Tabora;

vii) Kuhuisha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya 2007;

viii) Kufuatilia matumizi ya fedha za umma katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ili kuhakikisha utekelezaji wake unazingatia thamani halisi ya fedha;

ix) Kutumia njia za mawasiliano za kimkakati kulifikia kundi la vijana ili washiriki katika shughuli zinazowajenga kimaadili na hivyo kujenga jamii inayochukia rushwa;

x) Kutoa mafunzo ya Stashahada ya Uzamili ya Uongozi “Postgraduate Diploma in Leadership” kwa lengo la kuwajengea uwezo viongozi katika maeneo ya kufanya maamuzi ya kimkakati, kusimamia raslimali watu na raslimali nyingine na kuimarisha sifa binafsi za kiongozi;

xi) Kuendelea kuratibu na kuwezesha timu za kitaifa za majadiliano ya mikataba yenye thamani kubwa kulingana na uhitaji;

xii) Kuanzisha vituo vitano vya urasimishaji biashara ili kuwawezesha wafanyabiashara kupata huduma muhimu sehemu moja katika halmashauri za wilaya tano za Kahama, Tabora, Nyamagana, Songea na Babati. Aidha, mafunzo ya kurasimisha na kuendesha biashara yatatolewa kwa wafanyabiashara 5000 kwa lengo la kuwawezesha kusajili biashara zao;

xiii) Kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa miradi ya majaribio ya Mfuko Endelevu wa Urasimishaji wa Wilaya katika Manispaa ya Iringa na Halmashauri ya Wilaya ya Njombe;

xiv) Kufanya utambuzi na uandikishaji wa kaya maskini zipatazo 355,000 katika vijiji 4,408, mitaa 1,189 na shehia 96, ambazo hazikufikiwa katika awamu ya kwanza;

xv) Kuhamasisha mamlaka zote 187 za utekelezaji wa mpango wa ruzuku kwa kaya maskini kuingia kwenye mfumo wa malipo ya walengwa kwa njia ya kielektroniki (kupitia mitandao ya simu na benki), ili kuwahisha malipo na kupunguza gharama za uendeshaji;

xvi) Kutoa huduma ya usafiri wa anga kwa viongozi wakuu wa kitaifa;

xvii) Kusimamia mikataba ya ukodishaji wa ndege kwa kampuni ya ndege ya taifa (ATCL);

xviii) Kusimamia ajira za watumishi wa umma ambapo katika mwaka wa fedha 2019/20 serikali inatarajia kuajiri watumishi wapya 57,807 wa kada mbalimbali na kupandisha vyeo watumishi 290,625 wa kada mbalimbali;

xix) Kuendelea na mchakato wa kutumia wa ujazaji wa fomu za matamko ya raslimali na madeni kwa viongozi wa umma kwa njia ya mtandao (*online application*) baada ya kukamilika kwa mfumo wa kielektroniki wa menejimenti ya taarifa za kimaadili *(ethics management information system* - *EMIS*);

xx) Kufanya uhakiki wa matamko ya raslimali na madeni kwa viongozi wa umma 2,000;

xxi) Kuandaa taarifa nne (4) za gharama za maisha kama msingi wa kukadiria kiwango cha mshahara wenye staha

ili kuwezesha kushauri kuhusu kiwango kinachoendana na gharama halisi za maisha;

xxii) Kufanya ukaguzi wa kawaida katika taasisi 150 na ukaguzi maalum katika taasisi 10 kwa lengo la kuangalia uzingatiaji wa sheria, kanuni, taratibu na miongozo ya usimamizi wa raslimali watu katika utumishi wa umma;

xxiii) Kukusanya taarifa na machapisho mbalimbali yanayohusu historia ya nchi yetu kutoka taasisi za umma na watu binafsi; na

xxiv) Kuimarisha mifumo ya kielektroniki katika usimamizi wa taarifa, kumbukumbu na nyaraka za taifa kwa kuhifadhi kumbukumbu na nyaraka katika teknolojia ya kisasa ya kidijitali (*digital records and archives management and preservation systems)* ili kurahisisha upatikanaji na kulinda nakala halisi.

**Mheshimiwa Spika,** ili iweze kutekeleza malengo hayo yaliyokusudiwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, inaomba kuidhinishiwa jumla ya **shilingi 683,529,211,617.** Kati ya fedha hizo **shilingi 483,661,966,000.** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, na **shilingi 199,867,255,617** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Aidha, katika fedha za matumizi ya kawaida, **shilingi bilioni 35.4** sawa na asilimia 7.31 ni kwa ajili ya mishahara na **shilingi bilioni 448.25** sawa asilimia 92.69 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba, bajeti inayoombwa kuidhinishwa katika mwaka ujao wa fedha imeongezeka kwa **shilingi 14,434,665,608** sawa na asilimia 2.16 ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa katika mwaka wa fedha 2018/19 ambayo ilikuwa **shilingi 669,094, 556, 009.**

Ongezeko hilo la fedha limebadili mwenendo wa bajeti ya ofisi hii kwa miaka miwili ya fedha iliyopita (2017/18 na 2018/19) ambapo bajeti ilikuwa ikipungua.

Aidha, kwa upande wa fedha za maendeleo, uchambuzi umebaini kwamba kiasi kinachoombwa kuidhinishwa nacho kimeongezeka kwa kwa **shilingi 3,893,894,617** sawa na asilimia 1.99 ikilinganishwa na kiasi cha **shilingi 195,973,361,000** kilichoidhinishwa katika mwaka wa fedha 2018/19.

Uchambuzi zaidi umebaini kwamba, ingawa ongezeko hilo limebadili mwenendo wa bajeti ya maendeleo ambayo imekuwa ikipungua kwa miaka miwili ya fedha iliyopita (2017/18 na 2018/19), bado kiasi kilichoongezeka ni kidogo ikilinganishwa na kiasi kilichoongezeka katika fedha za matumizi ya kawaida. Aidha, licha ya ongezeko, bajeti

ya maendeleo kwa mwaka ujao wa fedha ni takribani asilimia 51.12 tu ya bajeti ya maendeleo iliyoidhinishwa na Bunge katika mwaka wa fedha 2017/2018.

## 5.2 Uchambuzi wa Bajeti ya Wizara kwa kulinganisha na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka wa Fedha 2019/2020

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati ulifanya ulinganisho wa bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Uchambuzi umelenga kubaini ni kwa kiasi gani ongezeko la bajeti ya Taifa linaathiri mwenendo wa bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, katika mwaka ujao wa fedha. Ufafanuzi wa uchambuzi huo umetekelezwa kwa kutumia jedwali, asilimia, ulinganishaji na utofautishaji, na ili kurahisisha maelezo Kamati imetumia Chati. Katika uchambuzi huo mambo yafuatayo yalibainika:-

i) Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ambayo ni **shilingi bilioni 683** sawa na asilimia 2.06 ya

Bajeti yote ya Serikali ambayo kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo wa 2019/20 ni **shilingi bilioni 33,105;**

ii) Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2019/20 unaonesha ongezeko la bajeti kwa asilimia 1.93, ikilinganishwa na Mpango wa Bajeti kwa mwaka 2018/19; ilihali bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa mwaka wa fedha 2019/20 imeongezeka kwa asilimia 2.16 ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa katika mwaka wa fedha 2018/19;

iii) Mpango wa Maendeleo ya Taifa unaonesha ongezeko la asilimia 2.0 katika fedha za maendeleo, ambazo ni sawa na asilimia 37 ya bajeti ya Taifa kwa mwaka wa Fedha 2019/20, wakati bajeti ya maendeleo kwa Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ambayo ni sawa na asilimia 0.60 ya Bajeti ya Taifa, imeongezeka kwa asilimia 1.99 ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2018/19. Aidha, **Jedwali Na. 02** linafafanua zaidi juu ya ulinganisho baina ya maeneo hayo mawili.


**Jedwali Na. 02:** Ulinganisho wa Bajeti ya Ofisi ya Rais (UUB) dhidi ya Bajeti ya Taifa, kwa mwaka wa fedha 2019/20

| **BAJETI KUU YA TAIFA 2019/2020** | **BAJETI YA OFISI YA RAIS – UUB 2019/2020** |
|---|---|


| Mgawanyo | Bajeti Kuu (Tsh.Milioni) | Asilimia ya Jumla ya Bajeti kuu | Mgawanyo | Bajeti ya Wizara | Asilimia ya Jumla ya Bajeti ya Wizara |
|---|---|---|---|---|---|
| OC | 3,576,706 | 10.80 | OC | 448,258,391,640 | 65.58 |
| Deni la Taifa | 9,721,127 | 29.36 | - | - | - |
| Mishahara | 7,558,974 | 22.84 | Mishahara | 35,403,574,360 | 5.18 |
| Maendeleo | 12,248,602 | 37.009 | Maendeleo | 199,867,255,617 | 29.24 |
| **Jumla** | **33,105,409** | **100** | **Jumla** | **683,529,211,617** | **100** |

**Chanzo:** Mpango wa Maendeleo wa Taifa, na Randama ya Ofisi ya Rais – UUB kwa mwaka wa fedha 2019/2020

Aidha, matokeo ya ulinganisho wa Bajeti ya Taifa, dhidi ya Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora yanaoneshwa sawia kwa kutumia **Chati Mraba Na.01** na **Na. 02** kama ifuatavyo:-




**Chanzo:** Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2019/20




**Chanzo:** Randama ya Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mwaka wa fedha 2019/2020

## 6.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kupitia taarifa za ukaguzi wa miradi ya Maendeleo, taarifa za utekelezaji wa bajeti iliyopita na maombi ya makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka ujao wa fedha, Kamati inapenda kutoa maoni na ushauri kwa Serikali kama ifuatavyo: -

i) Serikali iongeze kiasi inachotoa kuchangia utekelezaji wa mpango wa kunusuru kaya maskini, kwani mchango wake ni mdogo sana. Tangu kuanza kwa mpango huu katika mwaka wa fedha 2013/2014, hadi taarifa hii inaandaliwa Serikali imechangia **shilingi bilioni 4.35** tu kati ya **shilingi bilioni 66.5** ilizopaswa kuchangia, sawa **asilimia** 6.54. kwa ufafanuzi ufuatao: -

**Jedwali Na. 03:** Mchango wa Serikali na kiasi ilichotoa

| Na. | Mwaka wa Fedha | Kiasi kilichoahidiwa (Tshs. Bilioni) | Kiasi kilichotolewa (Tshs. Bilioni) | Bakaa (Tshs. Bilioni) |
|---|---|---|---|---|
| 01. | 2013/14 | 18.50 | 3.00 | 15.50 |
| 02. | 2014/15 | 14.00 | 0.60 | 13.40 |
| 03. | 2015/16 | 14.00 | 0.00 | 14.00 |
| 04. | 2016/17 | 14.00 | 0.00 | 14.00 |
| 05. | 2017/18 | 3.00 | 0.75 | 2.25 |
| 06. | 2018/19 | 3.00 | 0.00 | 3.00 |
| | **Jumla** | **66.50** | **4.35** | **62.15** |

ii) Serikali iwezeshe wanufaika wa mpango wa ruzuku kwa kaya maskini walioamua kujiunga na Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF), kutumia kadi hizo kupata huduma ya matibabu nje ya maeneo waliyosajiliwa. Aidha, kadi hizo zitambuliwe kwenye Hospitali/Vituo vya Afya na Zahanati binafsi kama ilivyo kwa aina nyingine za bima za afya;

iii) Zoezi la kutambua na kuandikisha kaya maskini katika maeneo ambayo hayakufikiwa katika awamu ya kwanza ya mradi wa ruzuku kwa kaya maskini, lifanyike mapema ili kaya maskini katika maeneo hayo ziweze kunufaika. Takwimu zinaonesha kuna maeneo ya vijiji 4,408, mitaa 1,189 na shehia 96 ambayo hayajafikiwa na mpango;

iv) Serikali kupitia TASAF iandae utaratibu ambao utawezesha kuwaondoa walengwa wa mpango wa kunusuru kaya maskini ambao wamejenga uwezo wa kujitegemea kiuchumi kutoka katika mpango huo, ili watoe nafasi kwa kaya maskini ambazo haziko katika mpango huo kuingizwa na kuanza kunufaika. Aidha, utaratibu huu utawafanya wanufaika watambue kwamba, unufaika wao ni wa muda na mara wanapojimudu kiuchumi wanapaswa kuondoka katika mpango (*to graduate*);

v) Serikali iendelee kupunguza urasimu katika kuthibitisha Watumishi wa nafasi za uteuzi. Kamati imebaini kwamba, baadhi ya watumishi katika ofisi za umma wamekuwa

wakikaimu nafasi hizo kwa zaidi ya miaka miwili, kwa madai ya kusubiri upekuzi (*vetting)*. Hali hiyo inawavunja moyo watumishi hao na kuathiri utendaji wao kwani hushindwa kufanya maamuzi ya msingi;

vi) Halmashauri zitumie maafisa maendeleo ya jamii kuelimisha wanufaika wa mpango wa ruzuku kwa kaya maskini namna wanavyoweza kutumia sehemu ya ruzuku hiyo kujikwamua kiuchumi;

vii) Zoezi la kuhakiki na kuondoa kaya zisizo na sifa katika mpango wa ruzuku kwa Kaya maskini, litekelezwe kwa uangalifu ili kuepuka uonevu na malalamiko kutoka kwa waathirika;

viii) Serikali iongeze Mshahara kwa Watumishi wa Umma ili kuwawezesha kumudu gharama za maisha ambazo zinaongezeka kila kukicha. Sote ni mashahidi kwamba, Serikali haijaongeza mshahara wa watumishi wa umma kwa mwaka wa tatu sasa;

ix) Serikali iongeze bajeti ya MKURABITA na kutoa kikamilifu na kwa wakati fedha inayotengwa, ili kuongeza kasi ya upimaji na urasimishaji wa Ardhi na biashara za Wananchi. Hadi mwezi Februari, 2019 MKURABITA ilikuwa haijapokea fedha yoyote ya maendeleo kati ya **shilingi bilioni 1.5** zilizoidhinishwa na Bunge;

x) Watendaji wa Halmashauri washirikiane na MKURABITA, katika kuandaa na kutekeleza Mpango bora wa matumizi ya ardhi na

hivyo kupunguza au kuepusha migogoro ya ardhi baina ya makundi ya watumiaji katika jamii;

xi) Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania, Kampasi ya Mtwara kiwezeshwe kumiliki viwanja Na. 41 na 46 kwa ajili ya ujenzi wa mabweni na hivyo kuondoa usumbufu wa Wanafunzi wanaolazimika kuishi mbali na chuo hicho;

xii) Serikali kupitia Taasisi ya Uongozi (Uongozi Institute) iendelee kutoa mafunzo ya Uongozi na Utawala kwa Viongozi wanaoteuliwa ili kuwakumbusha juu ya umuhimu wa kuzingatia sheria, kanuni na miongozo ya kiutendaji na hivyo kuepusha migongano isiyo ya lazima. Kutolewa mafunzo hayo kumeanza kuzaa matunda ambapo vitendo vya ukiukwaji wa sheria za kiutendaji vimepungua; na

xiii) Kamati inapongeza juhudi za Serikali kupitia TAKUKURU za kushughulikia wala rushwa wakubwa kwa kuwafikisha mbele ya sheria. Hata hivyo, Kamati inashauri juhudi hizo pia zielekezwe kukabili vitendo vya rushwa ndogo ndogo zinazotendeka barabarani (askari polisi wa barabarani/madereva), hospitalini (madaktari na wauguzi) na mahakamani/mabaraza ya ardhi (waendesha mashitaka/makarani/mahakimu) n.k ambazo ni kero kwa wananchi. Aidha, Serikali iandae utaratibu wa kuingiza somo la maadili katika mitaala ya elimu ya msingi na sekondari ili kuandaa na kukuza kizazi chenye maadili na uzalendo.

## 7.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukupongeza wewe binafsi, kwa kuendelea kuliongoza Bunge hili vema na kwa weledi na umahiri wa hali ya juu. Nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Maoni ya Kamati kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa.

Napenda kumpongeza Mheshimiwa Naibu Spika, Dkt. Tulia Ackson, Mb, kwa umahiri wake katika kukusaidia kuongoza Bunge na Wenyeviti wa Bunge kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kukushauri na kukusaidia kuendesha vikao vya Bunge. Wote kwa pamoja tunawaombea afya njema katika kutekeleza majukumu mliyopewa.

Aidha, ninawashukuru kwa dhati Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, kwa ushirikiano wao katika kipindi chote cha uchambuzi wa bajeti ya ofisi hii ambao umewezesha kukamilika kwa taarifa hii. Ninaamini tutaendelea kushirikiana kikamilifu katika kutekeleza shughuli za Kamati, na hivyo kutimiza

wajibu wetu wa kuwawakilisha wananchi na kusimamia kikamilifu utekelezaji wa shughuli za Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati hii inashughulikia mafungu mengi ya bajeti (mafungu 36) na kwa kuzingatia muda mfupi uliotengwa wakati wa uchambuzi, ni wazi wajumbe walilazimika kufanya kazi kwa saa nyingi wakati mwingine hadi jioni kabisa. Hata hivyo, mazingira hayo hayakuwa kikwazo kwa namna yoyote kwao na badala yake walitekeleza jukumu la uchambuzi kwa moyo na weledi wa hali ya juu, ikiwa ni ishara ya utayari wao katika kuwatumikia Wananchi, Bunge na Taifa kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** kwa umuhimu wa namna ya pekee ningetamani sana kuwatambua Wajumbe wa Kamati kwa kutaja majina yao. Hata hivyo, kutokana na ufinyu wa muda naomba majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard). Majina hayo ni haya yafuatayo: -

1. Mhe. Dkt. Jasson Samson Rweikiza, Mb – Mwenyekiti
2. Mhe.Mwanne Ismail Mchemba,Mb –Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Margareth Simwanza Sitta, Mb,
4. Mhe. Angelina Adam Malembeka Mb
5. Mhe.George Malima Lubeleje,Mb
6. Mhe.Hamad Salim Maalim,Mb
7. Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Mb
8. Mhe.Innocent Sebba Bilakwate,Mb

9. Mhe.Mwatum Dau Haji,Mb
10. Mhe.Dkt. Saada Mkuya Salum,Mb
11. Mhe.Salum Khamis Salum,Mb
12. Mhe.Venance Methusela Mwamoto,Mb
13. Mhe. Anna Joram Gidarya, Mb
14. Mhe. Jerome Dismas Bwanausi, Mb
15. Mhe. Martha Moses Mlata, Mb
16. Mhe. Lusia Ursula Michael, Mb
17. Mhe. Mansoor Hilani Shanif, Mb
18. Mhe. Rehema Juma Migilla, Mb
19. Mhe. Joseph Roman Selasini, Mb
20. Mhe. Joel Mwaka Makanyaga, Mb
21. Mhe. Philipo Augustino Mulugo, Mb
22. Mhe. Ibrahim Hassanali Mohamedali Raza, Mb
23. Mhe. Khatib Said Haji, Mb
24. Mhe. Njalu Daudi Silanga, Mb
25. Mhe. Daniel Edward Mtuka, Mb
26. Mhe. Hamidu Hassan Bobali, Mb

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Kamati ninamshukuru Mhe. Kapteni Mstaafu George Huruma Mkuchika, (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Dkt. Mary Machuche Mwanjelwa (Mb), Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora kwa

ushirikiano wao kwa Kamati katika kipindi chote cha kutekeleza majukumu yake.

Nawashukuru pia watendaji wa wote wa ofisi hii wakiongozwa wakiongozwa na Makatibu Wakuu Dkt. Moses Kusiluka (Ikulu), Dkt. Lauren Ndumbaro (Utumishi), na Naibu Katibu Mkuu (Utumishi) Dkt. Fransic Michael kwa ushirikiano wao kwa Kamati wakati wa kupitia taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2018/2019, na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Aidha, shukrani zangu ziwaendee pia wakuu wa taasisi, idara na vitengo vilivyopo chini ya ofisi hii kwa ushirikiano wao kwa Kamati wakati wote wa utekelezaji wa majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndg. Stephen Kagaigai kwa kuiwezesha Kamati kukamilisha kazi yake bila kukwama. Aidha, namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Husein, Mkurugenzi Msaidizi, Ndg. Angelina Sanga, Makatibu wa Kamati Ndg. Chacha Nyakega na Ndg. Eunike Shirima, wakisaidiwa na Ndg. Modesta Kipiko, kwa kuratibu vizuri shughuli za Kamati ikiwa ni pamoja na kukamilisha maandalizi ya taarifa hii.

Vilevile, napenda kuwashukuru watendaji wote wa Kitengo cha Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard) wakiongozwa na Bi. Hanifa Masaninga kwa kuhakikisha taarifa hii inachapishwa kwa wakati na kwa ubora.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa mwaka wa fedha 2019/2020, kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Dkt. Jasson S. Rweikiza (Mb)
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA**
**NA SERIKALI ZA MITAA**
10 Aprili, 2019